## Ofisi ya Huduma za Biashara Mpakani (Trade Service Hubs)

Ofisi ya Huduma ya Taarifa za Biashara (*Trade Services Hub*) ni kituo cha taarifa za biashara mpakani ambacho kinaendeshwa na wafanyabiashara wanawake. Vituo hivi vinakusudiwa kuwepo katika mipaka ya Tanzania na nchi zinazopakana ili kuwezesha wafanyabiashara wa Wadogo na Kati (SMEs), kupata taarifa mbalimbali kuhusiana na uvushaji bidhaa mpakani hapo. Tanzania inavituo katika mipaka tisa (9) ambayo wafanyabiashara wanawake wameunda asasi za kuweza kuendesha ofisi hizo kwa msaada wa wahisani mbalimbali. Mipaka hiyo ni:-

- ✓ Mutukula (Tanzania/mpaka na Uganda)
- ✓ Namanga (Tanzania/ Mpaka na Kenya)
- ✓ Kabanga (Tanzania/Mpaka na Burundi);
- ✓ Rusumo (Tanzania/Mpaka na Rwanda);
- ✓ Manyovu (Tanzania/Mpaka na Burundi);
- ✓ Sirari (Tanzania/mpaka na Kenya);
- ✓ Tarakea (Tanzania/mpaka na Kenya);
- ✓ Holili (Tanzania/Mpaka na Kenya);
- ✓ Horohoro (Tanzania/Mpaka na Kenya).

Ofisi ya Huduma ya Taarifa za Biashara Mpakani (Women ICBT Trade Hubs) zitawezesha wafanyabiashara kufahamu taratibu mbalimbali za uvushaji bidhaa mpakani hapo na pia kusaidia upatikanaji wa nyaraka mbalimbali kwa wafanyabiashara wadogo wanaofika kuhitaji kuvuka mpaka wakiwa na bidhaa zisizozidi Dola 500 na 2000 za marekani. Kazi za ofisi hiyo ni pamoja na:

- ✓ Kuwawezesha kuongeza utii wa taratibu zilizopo mipakani;
- ✓ Kuwajengea ufahamu juu ya namna sahihi ya kuendesha biashara za kuvuka mipaka;
- ✓ Kuwawezesha na kurasimisha biashara za wanawake sekta isiyo rasmi kuwa katika mfumo rasmi wa biashara ya mpakani; biashara zisizo rasmi kuwa biashara rasmi
- ✓ Kuwawezesha kuunda vikundi vya biashara na tawala zake;
- ✓ Kusaidia uanzishwaji wa mafunzo ya biashara na uwezeshaji ili kuendeleza na kuimarisha biashara rasmi mipakani;
- ✓ Kuhamasisha maendeleo ya biashara ya bidhaa zinazopelekwa nje na kuingizwa ndani ya nchi;
- ✓ Uwezeshaji kufikia fursa za biashara nchi jirani kwa wafanyabiashara wanawake;
- ✓ Kuchangia utekelezwaji fasaha wa mpango na utaratibu uliorahisishwa kwa wafanyabiashara ndogo ndogo wa Afrika Mashariki.
- ✓ Kuongeza uelewa juu ya fursa na uwekezaji juu ya biashara za kuvuka mipaka kwa wanawake;
- ✓ Kuwashawishi wadau kuhusu kupunguza vikwazo vya biashara kwa wanawake ili kuongeza biashara baina ya mataifa ya EAC;
- ✓ Kusajiri na kuwezesha uundwaji wa mtandao wa wafanyabiashara wanawake mipakani katika nchi tunazopakana nazo.
- ✓ Kuwa kitovu cha mawasiliano baina ya asasi ya wafanyabiashara wanawake na serikali ya Halmashauri ya wilaya na Taasisi wezeshi kibiashara nchini.
- ✓ Njia rahisi ya Taasisi za Udhibiti Bidhaa Mpakani kuwafikia wafanyabiashara wa maeneo ya mpakani na kutoa elimu..



*Mkutano wa Trade Hub- OSBP Mpaka wa Mutukula*

### Huduma Zitolewazo na Trade Hubs

- ✓ Fursa za biashara kwa SMEs zipatikanazo nchi jirani;
- ✓ Kutoa ushauri wa kurasimisha bidhaa wanapovuka mpaka (border declaration);
- ✓ Kutoa ushauri wa taratibu za kuvuka mpaka na biashara ya mpakani;
- ✓ Ufundishaji wafanyabiashara ndogo ndogo mipakani na ushauri juu ya mambo yahusuyo upelekaji bidhaa nje ya nchi, taratibu zilizopo, uendeshaji na kuwajengea uwezo vikundi.
- ✓ Kusaidia upatikanaji wa taarifa za kodi na tozo za mamlaka muhimu katika urasimishaji wa biashara zisizo rasmi.

### Faida za Trade Hubs

Uanzishwaji wa Ofisi ya Huduma za Biashara (OHB) kwa wanawake ni wa manufaa kwa Serikali na wafanyabiashara ndogo ndogo wanao jihusisha na kuvuka mipaka:

Kwa Serikali itasaidia;

- ✓ Udhibiti wa majanga yanayowahusu wanawake hususani wa mipakani;
- ✓ Itaongeza hali ya usalama maeneo ya mpakani;
- ✓ Itaongeza mapato kutokana na malipo ya tozo mbalimbali kwa wafanyabiashara;
- ✓ Upatikanaji wa takwimu za wafanyabiashara ndogo ndogo mipakani;
- ✓ Serikali kutambua kiasi gani inasaidia wafanyabiashara wadogo katika juhudi za kupunguza umasikini nchini.
- ✓ Kupunguza gharama za miamala, kuongeza ushindani wa kibiashara, kupata taarifa na kuhakikisha usalama wa biashara.
- ✓ Kuimarisha Biashara ya Ushindani Soko la Afrika Mashariki.

Tanzania kuna vituo vya Forodha Mpakani "*One Stop Border Post (OSBP)*" saba ambapo viwili viliisha funguliwa vinaendelea na kazi, vingine vinaandaliwa ikiwemo cha Tunduma ambacho kinatazamiwa kujengwa.




*Katika kila ofisi ya OSBP TanTrade inaratibu utendaji wa Kamati za Pamoja Mipakani (Joint Border Committee - JBC) ili kubaini vikwazo katika kurahisisha mazingira ya uvushaji bidhaa mipakani na kufuatilia ufumbuzi juu ya matatizo yanayojitokeza katika urahisishaji mazingira ya biashara nchini. JBC inahusisha watendaji wote wa serikali walipo mpakani pamoja na mwakilishi toka WICBTA, TAFFA au TCCIA, na Afisa Biashara Wilaya katika vikao vyake.*



*Picha ya Pamoja ya Washiriki wa Mkutano wa Kituo cha Taarifa Mpakani Kabanga*

## Mawasiliano ya Viongozi wa Asasi za Wafanyabiashara Wanawake Mpakani Tanzania (Trade Services Hubs Offices)

**Mutukula Women Trade Services Hub**
Mutukula WICBT Association
Mwenyekiti: Bi. Saida Kassim
Simu: +255 (0)787 009 678/ 763 699 168

**Kabanga Women Trade Services Hub**
Kabanga WICBT Association
Mwenyekiti: Bi. Adelaida Majanja
Simu: +255 (0)784 203 177

**Rusumo Women Trade Services Hub**
Rusumo WICBT Association
Mwenyekiti: Bi. Verena Leodigard
Simu: +255 (0) 756 979 902

**Manyovu Women Trade Services Hub**
Manyovu WICBT Association
Mwenyekiti: Bi. Betha Matanwa
Phone: +255 (0) 765 142 516

**Sirari Women Trade Services Hub**
Sirari Women ICBT Association
Mwenyekiti: Bi. Penina N. Nyabusibai
Simu : +255 (0)752 235862
Barua pepe : Peninanyaisava@yahoo.com

**Namanga Women Trade Service Hub**
Namanga Women ICBT Association
Mwenyekiti: Bi. Grace Sebastiani Kira
Simu: +255 (0) 762087829
Barua pepe: gracekirah@3gmail.com

**Horohoro Woman Trade Services Hub**
Horohoro Women ICBT Association
Makamu M : Mariam Makoko
Simu: +255 (0)715 158594 / 712 183046

**Tarakea Woman Trade Service Hub**
Tarakea Women ICBT Association
Mwenyekiti : Bi. Editha Josephati
Simu: +255 (0) 784 680253

**Holili Woman Trade Services Hub**
Holili Women ICBT Association
Mwenyekiti: Bi. Germana Opundo
simu: +255 (0)754 065277

# KITUO CHA HUDUMA ZA BIASHARA MPAKANI WOMEN TRADE SERVICES HUBS -TANZANIA-

**Uendelezaji Wafanyabiashara Wanawake (SMEs) Afrika Mashariki ili kuwawezesha kukidhi vigezi vya kuvusha Bidhaa Mipakani kwa njia iliyo rasmi**




Mkurugenzi Mkuu
**Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania,**
S. L. P 5402, DAR ES SALAAM. Tanzania
Tel: +255 22 2850238 / 2850065
Barua pepe: info@tantrade.go.tz

*"TanTrade, Kwa Ukuzaji wa Biashara"*